JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

HOTUBA YA MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI (MB.) WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA), KUMKARIBISHA MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHE. SAMIA SULUHU HASSAN, KATIKA KUADHIMISHA SIKU YA MAADILI KITAIFA NA HAKI ZA BINADAMU,
TAREHE 10 DESEMBA, 2016

VIWANJA VYA MNAZI MMOJA - DAR-ES-SALAAM

Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
Mhe. *Dkt.* Harrison G. Mwakyembe (Mb.), Waziri wa Mambo ya Katiba na Sheria;
Mhe *Dkt.* Phillip Mpango (Mb.), Waziri wa Fedha na Mipango;
Mhe *Prof.* Joyce Ndalichako (Mb.), Waziri wa Elimu, Satyansi na Teknolojia;
Mhe *Prof.* Makame Mbarawa (Mb.), Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano;
Mhe. George Masaju Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
Mhe. *Dkt.* Medard Kalemani (Mb.) Naibu Waziri wa Nishati na Madini;
Mhe. *Eng.* Edwin Ngonyani (Mb.) Naibu Waziri wa Ujenzi, uchukuzi na Mawasiliano;
Mhe. *Eng*. Isack Kamwelwe (Mb.) Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji;
Mhe. Mhe. Jaji Ferdinand Wambali, Jaji Kiongozi;
Mhe: Paul Makonda, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;
Mratibu wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Maendeleo (UNDP) nchini, Mhe. Alvaro Rodrigues;
Bw. Valentino Mlowola, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Maadhimisho haya;
Mhe. Jaji (Mst.) James Bwana, Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Umma;
Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu;
Wakuu wa Taasisi walioshirikiana kuandaa maadhimisho haya;
Watumishi wa Umma mliopo hapa;
Viongozi wa Dini na Siasa;
Ndugu Wanahabari,
Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana.

Asalaam Aleikhum, Bwana Asifiwe, Tumsifu Yesu Kristo,

Kwanza kabisa nianze kwa kukushukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa kukubali kujumuika nasi siku ya leo kwenye maadhimisho ya siku ya Maadili na Haki za Binadamu. Tunatambua jinsi ulivyokabiliwa na majukumu mengi ya kitaifa lakini bado umeweza kuwa nasi asubuhi hii. Tumefajirika sana na uwepo wako hapa siku ya leo. Karibu sana Mheshimiwa Makamu wa Rais.

Pili, naomba nitumie fursa hii na mimi kuongeza kauli yangu kuwakaribisha na kuwashukuru Viongozi na Wananchi mliojumuika nasi kwa wingi hapa leo. Tunatambua leo ni siku ya mapumziko na wengi wenu mna majukumu mbalimbali ya kitaifa yanayowakabili, lakini mmeweza kutenga muda wenu kuadhimisha siku hii muhimu kwa nchi yetu. Karibuni sana.

Tatu, napenda kuwapongeza wote walioshiriki na kuchangia kwa namna moja au nyingine kufanikisha siku hii. Ninatambua mchango mkubwa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupamabana na Rushwa, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali, Mamlaka ya Udhibiti na Manunuzi ya Umma, Tume ya Utumishi wa Umma na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Vilevile, ninatambua mchango mkubwa wa Vyombo vya Habari vikiwemo vyombo vya TBC, ITV, AZAM TV, eFM redio, Magic FM, Clouds FM na TBC Taifa, Azam Redio, Redio One pamoja na magazeti mbalimbali. Kwa hakika, ushirikiano wa wadau wote na moyo wao wa kujitoa katika kipindi chote cha Mwezi wa Maadhimisho ya Siku ya Maadili Kitaifa na Haki za Binadamu ni wa kupigiwa mfano. Tunawashukuru na kuwapongeza sana.

Mheshimiwa Makamu wa Rais,

Mbali na wadau niliowataja, wapo wadau wengine waliotuunga mkono kwenye maadhimisho haya ningependa kuwatambua. Wadau hao ni pamoja na Mfuko wa Uwekezaji wa Taifa (UTT), Mfuko wa Bima ya Afya wa Taifa (NHIF) na Kitengo cha Damu Salama cha Taifa (Muhimbili). Kupitia wadau hawa Wananchi walipata elimu kuhusu Bima ya Afya na

uwekezaji na pia fursa kujiunga na huduma hizo. Aidha, Wananchi pia walipata fursa ya kupima afya zao, kupata ushauri wa kitaalam bure na Kuchangia Damu kwa hiyari. Tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Makamu wa Rais,

Pamoja na dhumuni kuu la kuadhimisha siku ya Maadili Kitaifa na Haki za Binadamu, siku ya leo tunahitimisha Kampeni ya Kujenga na Kukuza Maadili, Haki za Binadamu, Uwajibikaji, Utawala Bora na Mapambano dhidi ya Rushwa, ambayo ilizinduliwa Rasmi tarehe 10 Novemba, 2016. Katika kipindi chote hicho, shughuli mbalimbali zimefanyika ikiwa ni pamoja na Kuendesha Wiki ya Huduma kwa Wananchi, Kufanya Matembezi ya Hiyari pamoja na kuendesha Midahalo.

Ninawapongeza wote walioshiriki kwenye shughuli hizo na kipekee ninatambua ushiriki wa Viongozi waliotuzindulia shughuli hizo akiwemo Mhe. *Prof.* Joyce Ndalichako (Mb) Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, aliyezindua mdahalo, Mheshimiwa *Dkt.* Harrison Mwakyembe (Mb) Waziri wa Mambo ya Katiba na Sheria aliyezindua Wiku ya Huduma kwa Wananchi na Mhe. *Mhandisi Balozi* John Kijazi, Katibu Mkuu Kiongozi aliyeongoza Matembezi ya Hiyari. Ninawashukuru sana.

USHIRIKIANO WA TAASISI KWENYE MAADHIMISHO YA MWAKA HUU

Mheshimiwa Makamu wa Rais,

Mwaka huu tulifanya uamuzi wa makusudi wa kuuganisha maadhimisho ya Siku ya Maadili na Siku ya Utawala Bora. Uamuzi huu umetokana na sababu mbalimbali. Mojawapo ni kupunguza gharama. Kwa kufanya hafla kwa pamoja, tumejikuta tukiua ndege wawili kwa jiwe moja. Lakini pia, ipo sababu nyingine ya msingi zaidi. Maadili na Utawala Bora ni mambo mawili yanayoshabihiana sana.

Kwa mfano, sote tunafahamu kwamba ili TAKUKURU ipate ufanisi katika utendaji wake wa kazi, haina budi ifanye kazi kwa ushirikiano wa karibu na taasisi zinazohusika na maswala ya sheria, utoaji wa haki na utawala bora. TAKUKURU haiwezi kufanikiwa katika shughuli zake kama haitakuwa na mahusiano mazuri na ushirikiano wa karibu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG Chambers), Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (PPRA)na taasisi nyinginezo. TAKUKURU inazihitaji taasisi hizi kama ambavyo kila moja ya taasisi hizi nazo zinavyoihitaji TAKUKURU kwa ukamilifu wa shughuli zake.

Kutoshirikiana ipasavyo kwa vyovyote vile kunadhoofisha dhamira ya Serikali ya kujenga utawala bora. Hivyo tuliona tuungane pamoja kwenye maadhimisho ya mwaka huu kwani hata wahenga walisema UMOJA NI NGUVU NA UTENGANO NI UDHAIFU.

Ndugu Wananchi,

Ninaposema haya, naomba isieleweke kwamba hapakuwepo ushirikiano miongoni mwa taasisi zetu. La hasha! Ushirikiano umekuwepo siku zote. Kwa mfano, TAKUKURU inayo makubaliano ya ushirikiano na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) katika kushughulikia masuala ya rushwa katika ununuzi wa bidhaaa na huduma Serikalini. Hatua hii imezingatia hali halisi kwamba rushwa nyingi na hasa zile kubwa kubwa Serikalini zinahusiana na shughuli za ununuzi wa mahitaji ya Serikali na mikataba mbalimbali ya huduma n.k. Hatua hii pia imesaidia kuhakikisha kuwa fedha za Umma zinadhibitiwa ipasavyo na kutumika kufanya kazi iliyokusudiwa ya kuwahudumia Wananchi wapate maendeleo na kuboresha maisha yao. Vivyo hivyo,kupitia taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, TAKUKURU wameweza kupata taarifa muhimu za kufanyia kazi katika mapambano dhidi ya rushwa.

Mheshimiwa Makamu wa Rais,

Siku ya leo pia tunazindua Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu (yaani National Anti- Corruption Strategy and Action Plan – NACSAP III).

Mkakati huo utakaouzindua muda si mrefu umedhamiria kupunguza rushwa katika nyanja zote kwa kufanya yafuatayo:

(i) Kuweka Kipaumbele kwa sekta na maeneo yenye mazingira shawishi kwa rushwa;

(ii) Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Sheria za MAPAMBANO dhidi ya RUSHWA;

(iii) Kuimarisha na kuwezesha Umma kushiriki, kudai haki na uwajibikaji wa SERIKALI;

(iv) Kuimarisha Elimu ya Maadili na Mapambano dhidi ya Rushwa kupitia Mkakati wa Habari na Mawasiliano;

(v) Kuimarisha ubia na ushirikiano miongoni mwa Serkali na wadau mbalimbali (Mahakama, Bunge, na Asasi zisizo za Kiserikali, nk) katika mapambao dhidi ya Rushwa;

(vi) Kuimarisha na kuboresha mifumo ya utawala wa vyombo vya utoaji haki;

(vii) Kuimarisha na kujenga uwezo wa Taasisi Simamizi za Mapambano dhidi ya rushwa;

(viii) Kuweka Mkazo katika Matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma;

(ix) Kukuza uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa Shughuli za Umma;

(x) Kuingiza Elimu ya Maadili kwenye mitaala na mifumo ya elimu;

(xi) Kuimarisha Mifumo ya Tathmni ya ufuatiliaji katika utekelezaji wa Mikakati;

Mheshimiwa Makamu wa Rais,

Kwa kuhitimisha, naomba nikuhakikishie kwamba Taasisi za Uwajibikaji zina ari na zitaendelea na Mapambano dhidi ya Rushwa, Kusimamia manunuzi ya Umma, Kudhibiti Ubadhirifu wa fedha na Mali za Umma, Kuhakikisha kuna uzingatiaji wa Maadili kwa Viongozi wa Umma na Watumishi wa Umma, Haki za Binadamu zinaheshimiwa na Kulindwa,Taratibu za Utumishi wa Umma na Usimamizi wa Rasilimali Watu zinafuatwa, na dhana nzima ya Utawala Bora na Uwajibikaji inatekelezwa.

Baada ya kusema hayo MHE. MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWA HESHIMA NAOMBA KUKUKARIBISHA SASA UZUNGUMZE NASI TUPO TAYARI KUKUSIKILIZA.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA.